**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA**

**Tovuti: www.hlpc.go.tz**

# TANGAZO

**KUFANYIKA KWA ZOEZI LA UTATHMINI (COMPETENCY ASSESSMENT) KWA WAPIMAJI WA VVU WASIOKUWA WATAALAM WA MAABARA KUANZIA TAREHE 18-29 JULAI 2022**

Baraza la Wataalam wa Maabara kwa kushirikiana na mdau wa maendeleo (MDH) linachukua nafasi hii kuwatangazia wapimaji wa VVU wasiokuwa Wataalam wa Maabara ambao walipata mafunzo ya upimaji wa virusi vya Ukimwi kwa njia ya mtandao (ECHO) na kukidhi vigezo vya kufanyiwa tathmini kuwa;

1. Zoezi la utathmini litafanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itakuwa kuanzia tarehe 18 mpaka 22 mwezi Julai 2022 na awamu ya pili itaanza tarehe 25 mpaka 29 mwezi Julai 2022.

2. Wapimaji waliokidhi vigezo kufanyiwa tathmini wanatakiwa kujiandaa kwa zoezi katika vituo vyao husika wakiwa na picha mbili (passport size) kwa ajili ya kutengenezewa Leseni za upimaji.

3. Baraza linasisitiza wapimaji wanaofanyiwa tathmini kutunza namba zao za mitihani watakazopatiwa kwani matokeo hayatatoka kwa majina.

Ofisi ya Msajili inawasisitiza Wapimaji wote wanaotarajia kufanyiwa tathmini kuzingatia maelekezo.

Mawasiliano Simu: 0734005777, Email: **hlpc@afya.go.tz**

Imetolewa na:

..............................
Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara.